TANGAZO LA SERIKALI NA. 148 la tarehe 15/2/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI ZA MWAKA, 2019.

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana Kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi za Mwaka, 2019 na zitaanza kutumika mara zitakapotangazwa katika Gazeti la Serikali. *Jina na Tarehe ya kuanza kutumika.*

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi *Matumizi*

3. Katika Sheria Ndogo hizi maneno yafuatayo yatakuwa na tafsiri kama inavyoonekana hapa chini- *Tafsiri*

"Ada na Ushuru "maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa ajili ya Huduma vibali na Leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;
"Afisa Mwidhiniwa" Maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

'Bajaji' ni pikipiki yenye magurudumu matatu yenye uwezo wa kubeba abiria watatu na dereva;

"Boda Boda" maana yake ni Pikipiki zitumiazo magurudumu mawili (motocycle) zenye uwezo wa kubeba abiria mmoja na dereva;

"CBD" (Central Busines District) maana yake ni eneo la katikati ya Mji wa Moshi kama lilivyoanishwa katika

Mpango Kabambe wa mwaka 2001 linalojumuisha Kata za Mawenzi, Kiusa, Bondeni na sehemu ya eneo la Kata ya Korongoni linalotakiwa kujengwa maghorofa na sio vinginevyo;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Moshi;

"Kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali cha ujenzi kinachotolewa na Halmashauri chini ya Kanuni za Uendelezaji Miji za Mwaka 2008 zilizotungwa chini ya Sura Namba 288 na au Kanuni zilizofanyia mabadiliko kanuni hizo na au Sheria ndogo hizi;

"Maeneo ya Kati" maana yake maeneo yaliyopo katikati ya Mji yaani "Central Business District (CBD)";

"Mkurugenzi Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote yule ambaye atakuwa anatekeleza majukumu Mkurugenzi;

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru ulioorodheshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi kwa huduma, vibali na Leseni zitolewazo na Halmashauri.

(2) Ada na Ushuru itozwao chini ya Sheria Ndogohizi inapaswa kulipwa kabla ya mlipaji kupata huduma au leseni au kibali husika na kwa vyovyote vile haitazidi tarehe 30 ya mwezi wa Juni ya mwaka unaolipwa.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubadilisha viwango vya Ada na Ushuru muda wowote kadri itakavyoona kuwa inafaa kufanya hivyo.

Wajibu wa kulipa ada na Ushuru

5. Utakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa Ada na Ushuru, kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kulipa Ushuru na au Ada kama zilivyoelekezwa kwenye Jedwali la kwanza.

Ada na Ushuru

6. (1) Ada na Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake

ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha kukubali malipo hayo. kulipwa Halmashauri

(2) Hautakuwa ni utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mtu yeyote kudai kuwa amelipa Ada na Ushuru lakini hakupewa stakabadhi.

Kufifilisha kosa

7. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa katika Jedwali la Pili Sheria Ndogo hizi na kulipia Ushuru wa Mifugo pamoja na faini anayodaiwa isiyopungua kiasi cha shilingi laki mbili (Tsh. 200,000) na isiyozidi kiasi cha shilingi laki tano (Tsh.500, 000).

Ilani

8. (1) Mtu yeyote ambaye atashindwa kutekeleza maagizo yoyote yatakayotolewa kwenye Ilani na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

(2)Bila kujali mashartiyaliyomo kwenye kifungu Kidogo cha 8(1) cha Sheria Ndogo hizi ni kosa kwa mtu yeyote kutotii Ilani iliyotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria hizi Ndogo hizi.

Makosa na Adhabu

7. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kutumikia kifungu kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Sheria Zilizofutwa

10. Sheria Ndogo hizi zitafuta-

(a)Sheria Ndogo za (Ada ya Maegesho ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Mwaka 2005, GN No 211

(b) Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi za Mwaka 2006 GN. No 25.

JEDWALI LA KWANZA

( LIMETUNGWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 NA 5 )
SEHEMU :A
ADA ZA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ukumbi wa Halmashauri | 100,000/= kwa siku |
| 2. | Viwanja vya Halmashauri | 300,00/= hadi 2000,000 /==kwa siku kulingana na maboresho |
| 3. | Viti | Viti vidogo shilingi 500/=-kwa siku na viti vikubwa shilling1000/= kwa siku. |
| 4. | Lori | 100,000/= kwa siku |
| 5. | Tingatinga(wheel loader,grader,roller | 100000 /=kwa saa |
| 6. | Miambo mingine midogo | 50000/= saa |
| 7. | Nyumba za kuishi ambazo si watumishi | Kwa mujibu wa mkataba |

SEHEMU: B
ADA ZA KUPIMA AFYA KWA WAHUDUMU

| Na | Aina ya homa | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Kupima homa ya tumbo | Sh,7500/= |
| 2 | Kupima mkojo | Sh 5000/= |
| 3 | Kupima kaswende | Sh75000/= |
| 4 | Kupima haja kubwa | Sh.2000/= |
| 5 | Kupima homa zisizotajwa | Sh.3000/= |
| 6 | Kupima vipimo vilivyotajwa kwa mkupuo | Sh 10,000/= |

SEHEMU :C
ADA YA KUPULIZA DAWA YA WADUDU

| Na | | |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kupuliza dawa ya wadudu (Furmagation) ambayo itafanywa na Halmashauri | Sh.1000/= kwa mita moja (1) ya Mraba |
| 2 | Ada ya usimamizi wa kunyunyizia dawa ya wadudu inaofanywa na watu binafsi | Sh.50,000/= kwa kazi |
| 3 | Ada ya kupiga/kunyunyiza dawa kwa mtu mwenye dawa yake anayepigiwa na watumishi wa Halmashauri | Sh.500/= kwa kwa mita moja (1) ya mraba |

SEHEMU: D
ADA YA UKAGUZI

| Na | Aina ya sehemu | Kiwango cha ukaguzi |
|---|---|---|
| 1 | Hoteli | Sh. 30,000/=kwa mwaka |
| 2 | Mgahawa/baa | Sh.20,000/= kwa mwaka |
| 3 | Nyumba za kulala wageni | Sh.20,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Viwanda | Sh.50,000/= kwa mwaka |
| 5 | Biashara nyinginezo | Sh.10,000/= kwa mwaka |
| 5 | Ukaguzi wa dharura | Sh.20,000/= kwa mwaka |

SEHEMU: E.
ADA YA UZOAJI TAKA

| Na | Eneo la uzoaji | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Shopping Malls | Sh.1,200,000/= kwa mwaka |
| 2 | Uchafuzi kutokana na Maazimisho | Sh.1,200,000/= kwa Azimisho |
| 3 | Hospitali za Rufaa (Binafsi) | Sh.1,200,000/= kwa mwaka |
| 4 | Viwanda vikubwa /taasisi za kibenki na vyuo | Sh.780,000/=kwa mwaka |
| 5 | Hospital ya wlaya na za binafsi | Sh.600,000/=kwa mwaka |
| 6 | Hoteli ya utalii | Sh.420,000/=kwa mwaka |
| 7 | Shule ya bweni binafsi | Sh.360,000/=kwa mwaka |
| 8 | Hoteli ya kawaida | Sh.300,000/=kwa mwaka |
| 9 | Viwanda vidogo | Sh.260,000/=kwa mwaka |
| 10 | Baa na mgahawa | Sh.240,000/=kwa mwaka |
| 11 | Shule ya kutwa binafsi | Sh.240,000/=kwa mwaka |
| 12 | Nyumba za kulala wageni | Sh.180,000/=kwa mwaka |
| 13 | Vituo vya mafuta | Sh.180,000/=kwa mwaka |
| 14 | Duka la vifaa vya ujenzi,jumla ,duka la vipuri vya magali | sh.120,000/= kwa mwaka |
| 15 | Zahanati na vituo vya afya binafsi na maduka ya madawa | Sh.120,000/= kwa mwaka |
| 16 | Kalakana za mbao na duka la samani | Sh.120,000/= kwa mwaka |
| 17 | Hosteli binafsi zilizopo nje ya shule | Sh.120,000/= kwa mwaka |
| 18 | Kukodi gari la taka ya manispaa | Sh.100000/= kwa safari |
| 19 | Migahawa (Cafe, Ice cream, Tea & Studio room) | Sh.60000/= kwa mwaka |
| 20 | Maduka ya rejareja/Kinyozi/wauzamkaa/Sehemu maalum za kufulia na kunyosha nguo (*Dry cleaner*s)na Mabucha | Sh.60000/= kwa mwaka |
| 21 | Biashara nyinginezo | Sh.36000/= kwa mwaka |
| 22 | *Masoko/ Kituo cha Mabasi kwa SafariKaya* | Sh.15000/=kwa safari |
| 23 | *Magari* ya mizigo na mabasi | Sh.5000/=kwa safari |
| 24 | Ada ya kutupa taka sehemu ya kutupa taka*(Dampo* | Sh.15000/=kwa tani |

SEHEMU: G
ADA YA UNYONYAJI MAJI MACHAFU KWA
KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

| | Eneo | Kiasi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Maeneo ya biashara | Sh.40000/= kwa safari moja |
| 2 | Maeneo ya makazi | Sh.40000/= kwa safari moja |
| 3 | Nje ya eneo la Halmashauri | Sh.60000 /=kwa safari |
| 4 | Ngongeza kwa kutoka nje ya eneo la Halmashauri | Sh.3000/= kwa kila kilometa inayozidi mara baada ya kutoka eneo la Hlmashauri. |

SEHEMU:H
ADA YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI

| | Shughuli | kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Makazi kuwa kiashara | Sh.200000/= |
| 2 | Makazi kuwa viwanda | Sh.250000/= |
| 3 | Biashara kuwa viwanda | Sh.250000/= |
| 4 | Kugawanya kiwanja au shamba | Sh.50,000/= |
| 5 | Kubadili miliki kwa maeneo yasiyo na Hati | Sh.50,000/= |
| 6 | Mabadiliko mengine ambayo matumizi hayajatajwa | Sh.50,000/= |

SEHEMU :I
ADA ZA MAEGESHO NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

| Na. | Aina ya gari | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Taksi | Sh. 120,000/= kwa mwaka |
| 2 | Mabasi madogo ya abiria 25-30 | Sh.1500/= kwa safari |
| 3 | Mabasi makubwa | Sh.2,000/= kwa safari |
| 4 | Mabasi ya mzunguko mjini | Sh.1500/= kwa safari |
| 5 | Lori tani 2-5 | Sh.180,000/= kwa mwaka |
| 6 | Lori zaidi ya tani5 kwa maeneo yaliyotengwa na Manispaa | Sh.5,000/= kwa siku |
| 7 | pickup | Sh.180,000/= kwa mwaka |
| 8 | Magari yasiyokuwa ya biashara yanayoegeshwa katika maeneo ya mjini | Sh.1,000/= kwa siku |
| 9 | Kibali maalum cha kuegesha | Sh.40,000/= kwa mwezi |
| 10 | Kibali maalum cha kuhodhi maegesho | Sh.300,000/= kwa mwezi kwa kupande “slot” au sh .12,000/= kwa kipande “slot” itakapoegeshwa kila siku |
| 11 | Ada ya usajili magari ya biashara | Sh.15,000/= kwa mwaka |
| 12 | Ada ya kuegesha pikipiki | Sh.20,000/= kwa mwaka |

SEHEMU :J
ADA YA KUZINGIRA NA KUWEKA MAJUKWAA KATIKA MAENEO YA KATI NA MAENEO MENGINEYO KUTEGEMEA NA UKUBWA

| | Muda | Maeneo ya kati | Maeneo mengineyo |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Chini ya wiki 2 | Sh. 1,000/- kwa mita | Sh. 600/= kwa mita |
| 2 | Kati ya wiki 2 na 4 | Sh. 3,000/=kwa mita | Sh. 2,000/= kwa mita |
| 3 | Kati ya wiki 4 na 9 | Sh. 4,000/=kwa mita | Sh. 3,000/=`kwa mita |
| 4 | Kati ya wiki 9 na12 | Sh. 5,000/- kwa mita | Sh. 4,000/=-kwa mita |
| 5 | Kati ya wiki 12 na 52 | Sh. 8,000/= kwa mita | Sh. 7,000/= kwa mita |
| 6 | Zaidi ya mwaka | Sh. 10,000/= kwa mita | Sh. 9,000/= kwa mita |
| | | | |

SEHEMU:K
USHURU WA MASOKO NA MAGULIO

| Na. | Aina ya bidhaa | Kiwango cha ushuru kwa siku |
|---|---|---|
| 1 | Nyanya kilo 50 | Sh.400/= |
| 2 | Samaki kilo 50 | Sh.400/= |
| 3 | Mahindi kilo 100 | Sh.400/= |
| 4 | Mihogo,viazi vitamu,machungwa,nazi kilo 100 | Sh.400/= |
| 5 | Mchele ,ngano kilo 100 | Sh.600/= |
| 6 | Mpunga kilo100 | Sh.400/= |
| 7 | Vitunguu aina zote kilo 100 | Sh.700/= |
| 8 | Ndizi mbivu chini ya kilo 100 | Sh.200/= |
| 9 | Karoti kilo 100 | Sh.500/= |
| 10 | Ndizi mbichi chini ya kilo 100 | Sh.200/= |
| 11 | Maharage Dengu, Kunde | Sh.600/= |
| 12 | Ushuru wa mboga au matunda mengine chini ya kilo 100 masoko ya Mbuyuni, Kiusa, Soko Kuu, Kiborloni n.k | Sh.150/= |
| 13 | Ushuru wa matunda matunda yenye uzito chini ya kilo100 masokoni na vitu vingine ambavyo havikutajwa hapo juu, utatozwa | Sh.200/= |
| 14 | Ushuru kwa matumizi ya meza au kizimba | Sh.1000/= |

SEHEMU : L
ADA YA KIBALI CHA UJENZI KWA MWAKA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Maombi mapya ya ; | Kiasi kwa eneo la ujenzi |
| | Makazi | Sh. 400/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Makazi na biashara | Sh. 500/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Viwanda | sh. 400/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Taasisi | Sh. 300/=kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |

| | | |
|---|---|---|
| | Vituo vya mafuta | Sh. 600/= kwa kila mita1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| 2. | Maombi baada ya muda wa kibali wa mwaka mmoja kuisha; | |
| | Makazi | sh. 400/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Makazi na biashara | Sh. 500/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Viwanda | Sh. 400/= kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Taasisi | Sh. 300/=kwa kila mita 1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| | Vituo vya mafuta | Sh. 600/= kwa kila mita1 za mraba ya eneo la ujenzi |
| 3 | Maombi ya kukarabati nyumba; | |
| | Nyumba kawaida iliyoko pembezoni mwa mji na sio katika eneo la CBD | Sh.50000/= |
| | Nyumba ya ghorofa pembezoni mwa mji na katika eneo la CBD | Sh.100000/= |
| 4 | Kibali cha ujenzi wa nguzo ya kushikilia au ya kutumika katika kubandikwa kwa tangazo la biashara | Sh.100000/= |
| 5 | Kibali cha ujenzi minara ya simu | Sh.500,000/= |
| 6 | Kibali cha kuvunja jengo katikati ya mji | Sh.500,000/= |
| 7 | Kibali cha kujenga nguzo ya kuwekea tangazo la biashara: | |
| | Nguzo ndogo yenye kipenyo cha chini ya futi moja. | Sh.100,000/= |
| | Nguzo kubwa yanye kipenyo zaidi ya futi moja | Sh.200,000/= |

SEHEMU:M
ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA YALIYOSIMIKWA, KUCHORWA KUCHAPISHWA NA KUBANDIKWA KATIKA ENEO LOLOTE LA HALMASHAURI

| Na | Aina | Kiwango |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kufanya matangazo ya sauti au kutangaza | Sh.50,000/= kwa siku |
| 2 | Matangazo na miziki inayotokana na shughuli za harusi na shughuli zinazofanana na hizo | Sh. 60,000/= kwa siku |

SEHEMU :N
ADA YA MACHINJIO NA UKAGUZI

| Na. | Aina | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya Uchinjaji/Machinjio | Sh.5,000/= kwa kila Ng'ombe<br>Sh.2,000/=kwa kila Nguruwe<br>Sh.1,000/=kwa kila Mbuzi/Kondoo |
| 2 | Ada ya ukaguzi | Sh.500/= kwa kila Ng'ombe<br>Sh. 500/= kwa kila Nguruwe<br>Sh.400/= kwa kila Mbuzi/Kondoo<br>Sh. 100/= kwa kila Kuku |

SEHEMU O
ADA YA KIBALI CHA KUCHIMBA/ KUKATA BARABARA NA GHARAMA YA KUREJESHA HALI ILIVYOKUWA AWALI

| | Aina ya barabara | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Barabara ya lami | 350,000/= kwa urefu wa mita moja ya eneo |
| 2 | Barabara ya udongo | 100,000/= kwa urefu wa mita moja ya eneo |
| 3 | Ada ya kufunga barabara kwa sherehe au kwa shughuli yoyote ambayo siyo msiba wala ya kidini | 50,000/= kwa siku |

SEHEMU:P
ADA YA MATUMIZI YA UWANJA (GROUND RENT) NA MAENEO YA WAZI NDANI YA ENEO LA HALMASHAURI KWA SHUGHULI ZA BIASHARA

| | Aina | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka kuzunguka Kituo Kikuu cha Mabasi | Sh. 45,000/= kwa mita moja ya mraba kwa mwezi |
| 2 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka na karakana za kutengenezea magari uwanja wa Jamhuri | Sh.960,000/= kwa mwaka |
| 3 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka kuzunguka Soko la Kati, Soko la Kiusa na Mbuyun | Sh.840,000/= kwa mwaka |
| 4 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka na karakana za kutengenezea magari uwanja maeneo ya Soko la mtaa wa Dar es Salaam | Sh.600,000/= kwa mwaka |
| 5 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka na karakana za | Sh.600,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| | kutengenezea magari katikati viwanja karibu na Machinjio ya Bomambuzi | |
| 6 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka na karakana za kutengenezea magari uwanja wa majengo shilingi | |
| 7 | Ada ya kuendesha biashara ya maduka na karakana za kutengenezea magari katika masoko ya Kiborloni, Pasua Bomambuzi na maeneo mengine ambayo hayajatajwa s | Sh.360,000/= kwa mwaka |
| 8 | Ada ya kuendesha biashara iliyoruhusiwa katika maeneo ya wazi itakuwa kama itakavyotathminiwa na Mthamini na mkadiriaji wa majengo kwa thamani ya mita moja ya mraba katika eneo husika. | Sh180,000/= kwa mwaka |

SEHEMU:Q
ADA ZA KUPIGA PICHA, KUTUMIA FARASI KWENYE SHEREHE NA ADA YA KUMBI ZA STAREHE NA SHEREHE

| Na. | Aina | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kupiga picha katika bustani za Manispaa | Sh.50,000/= |
| 2 | Ada ya kupiga picha katika mizunguko inayomilikiwa na Manispaa | Sh.20,000/= |
| 3 | Maombi ya kibali cha kutumia Farasi katika sherehe kwa sherehe au shughuli | Sh.50,000/= |
| 4 | Maombi ya kibali cha kufanya Sherehe katika Ukumbi kutoka kwa Mmiliki kwa Tukio | Sh.60,000/= |
| 5 | Ushuru kutokana na kufanya shughuli katika sherehe utakaokusanya na mwenye ukumbi kwa niaba ya Halmashauri kutoka kwa; | |
| | Mpambaji wa sherehe | Sh.50,000/=kwa tukio |
| | Muandaaji wa chakula na vinjwaji | Sh.50,000/=kwa tukio |
| | Mshereheshaji wa sherehe | Sh.30,000/=kwa tukio |
| | Mpiga picha wa sherehe | Sh.20,000/=kwa tukio |
| | Mziki(dj) | Sh. 20,000/=kwa tukio |

SEHEMU: R
ADA YA BUSTANI ZA MAUA

| NA. | Aina ya bustani | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Vitalu vya miti | Sh.50,000/= kwa mwaka |
| 2 | Vitalu vya maua | Sh.50,000/= kwa mwaka |

SEHEMU : S
ADA YA KUWEKA NA KUTUMIA KIFAA CHA BIASHARA

| Na. | Aina ya biashara | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Cherehani | Sh.50000/= |
| 2 | Kutengeneza juice au chakula sehemu ya wazi | Sh.50000/= |

SEHEMU T
USHURU WA MATUMIZI YA CHOO

| | | |
|---|---|---|
| | Aina ya uduma | Kiasi |
| 1 | Haja ndogo na kubwa | 300 kwa awamu |
| 2 | Kuoga | 1000 kwa awamu |

JEDWALI LA PILI
( Limetungwa chini ya kifungu7 )

KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………… nakiri mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Manispaa ya Moshi kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka…... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za ( Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Moshi za Mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha deni ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ……………………………….

*Jina*……………………………….. *Saini*…………………..………………….

Mbele ya :
Jina: ……………………………………………
Cheo: ………………………………………….
Saini: ………………………………………….

Muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi uliobandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililotolewa kwenye kikao cha Mkutano wa Halmashauri kilichofanyika tarehe 27/04/2018 na kushuhudiwa na:

MICHAEL N. MWANDEZI
*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi*

NIMEKUBALI

RAYMOND R. MBOYA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa ya Moshi*

L.S

Dodoma,
…………., 2019

SELEMENI S. JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi-Or-Tamisemi*